HOMA YA NGURUWE (AFRICAN SWINE FEVER)

Na Augustino Chengula

Homa ya nguruwe ni ugonjwa unaoambukizwa kutoka nguruwe mmoja kwenda mwingine kwa kasi kubwa sana ukionyesha dalili mbalimbali. Dalili hizi zaweza kujionyesha dhahili au zisijionyeshe wazi wazi wakati huo ugonjwa ukiwa unasambazwa. Dalili ku inayoambatana na ugonjwa huu ni kuvuja na kusambaa kwa damu kwenye viungo vingi vya mwili wa mnyama.

Nguruwe wenye ugonjwa midomo yao ikiwa inavidonda

Nguruwe wenye ugonjwa wakiwa wamejikusanya pamoja wakiwa na vidoa doa vya damu

Masikio yakiwa mekundu kwa damu iliyoviria ndani ya ngozi

Kuvimba kwa figo zilizojaa damu



Madhara yake kwa nguruwe yanaweza kuwa makubwa au madogo yasiyoweza kuonekana kwa macho. Homa ya nguruwe haina tiba maalumu wala chanjo inayofaa na hivyo uzuiaji wa ugonjwa huu unategemea sana utambuzi wa ugonjwa mapema na kisha kuzuia utembeaji wa holela wa nguruwe (karantini). Maonyo yamekuwa yakitolewa kupitia mikutano ya hadhara na vyombo vya habari kama magazeti ya kuzuia kutembea kwa mifugo ovyo pamoja na kuzuia kula nyama ya nguruwe kwa kuhofia kusambaa kwa ugonjwa. Kiambatanisho Na 1 na 2 hapa chini vinaonyesha elimu iliyotolewa kwa mlipuko huo yaliyochapishwa na magazeti mawili tofauti kwa siku moja yakiashiria umuhimu wa ugonjwa huo.

Ugonjwa huu umekuwa ukitokea mara kwa mara katika nchi yetu na kuathiri mifugo na soko la nguruwe kwa ujumla. Ugonjwa huu uliripotiwa kwa mara ya kwanza

Tanzania mwaka 1914 ukifuatiwa na mlipuko mwingine mwaka ya 1962. Mlipuko mkubwa wa ugonjwa huu ulilipotiwa na Tasisi ya utafiti ya wanyama (ADRI), Dar es Salaam miaka ya 1987 an 1988 na kusababisha hasara kubwa sana kijamii na kiuchumi katika mikoa ya Mbeya, Arusha na Kilimanjaro. Tafiti zilizo fanywa na wataalamu wa magonjwa ya virusi (Misinzo na wenzake, 2011) kwa kutumia sampuli kutoka Chunya, Ileje, Kyela, Loliondo, Ludewa, Temeke and Tukuyu zilizokusanywa kati ya mwaka 2010 na 2011 wakati wa mlipuko zilionyesha kuwepo kwa ugonjwa maeneo hayo. Ugonjwa huu kwa nchi yetu umekuwa ukiripotiwa kama mlipuko ukianzia maeneo ya Mbeya ambako unaaminika kutoka nchi ya jirani ya Malawi. Mwezi may 2011, mlipuko wa ugonjwa pia ulilipotiwa Dar es Salaam nah ii inatokana na sababu kwamba Dar es Salaam sasa imekuwa na wafugaji wengi wa nguruwe kwa vile ufugaji wa nguruwe unaonekana kuwa na faida kubwa kwa mfugaji.

Kiambatanisho 1. **Nyama ya nguruwe yapigwa marufuku Mbeya** (http://www.freemedia.co.tz/daima/habari.php?id=22173) 22/12/2010

Na Moses Ng'wat, Mbeya

> SERIKALI mkoani Mbeya imetoa tahadhari kwa wananchi kuacha kula nyama ya nguruwe kutokana na kuingia kwa ugonjwa wa homa ya Nguruwe (African Swine Fever).
>
> Ugonjwa huo umeingia nchini ukitokea nchi ya jirani ya Malawi na tayari umeshaua nguruwe 328 katika wilaya za Rungwe na Kyela.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana mkuu wa mkoa wa Mbeya, John Mwakipesile, alisema ugonjwa huo umebainika takriban wiki moja baada ya kutokea tishio la ugonjwa huo katika nchi jirani ya Malawi.

Mwakipesile alisema serikali ilipata taarifa za kuzuka kwa ugonjwa huo kupitia vikao vya ujirani mwema ambavyo huambatana na kubadilishana taarifa.

Alisema ugonjwa huo ni hatari kwa afya za nguruwe ambapo mbali ya kuathiri wanyama hao lakini pia ni hatari kwa afya za binadamu.

“Baada ya kupata taarifa hizo, sisi kama jirani zao tulichukua tahadhari na baada ya wiki moja wataalamu wa wilaya za mpakani za Rungwe na Kyela nao wakabaini kuwepo kwa homa hiyo,” alisema Mwakipesile.

Alisema kwa mujibu wa taarifa alizozipata toka nchini Malawi ni kwamba serikali ya nchi hiyo iliamuru na kuendesha zoezi la kuteketeza nguruwe wote katika wilaya ya Kalonga iliyoko kusini mwa nchi hiyo ambayo inapakana na wilaya ya Kyela mkoani hapa.

Akifanunua juu ya hilo, mganga mkuu wa mifugo wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Solomon Ng’ong’ona, alisema licha ya ugonjwa huo kutokuwa na madhara yoyote kwa binadamu lakini ameshauri watu kutobweteka na kula nyama ya nguruwe ambaye amepatwa na ugonjwa huo.

Nong’ona alisema kuwa ugonjwa huo hauna tiba wala kinga.

Hivyo mbali na madhara ya kiafya kwa wanyama hao, pia ni hatari kwa madhara ya kiuchumi kwa kuwa wafugaji huweza kupoteza mifugo yao endapo hawatachukua hatua za kudhibiti.

Alizitaja dalili za ugonjwa huo kwa nguruwe kuwa ni kupata joto kubwa kutoka nyuzi joto 30 la kawaida hadi kuwa zaidi ya 40 na baada ya hapo hupenda kujikusanya pamoja, huku wakionyesha udhaifu.

Kiambatanisho 2. **Waonywa homa ya nguruwe Mbeya**

(http://www.mwananchi.co.tz/news/4-habari-za-kitaifa/7647-waonywa-homa-ya-nguruwe-mbeya.html)

Stephano Simbeye, Mbeya (22 December 2010)

SERIKALI mkoani Mbeya imewahadharisha wakazi wa mkoa huo kuacha kula ovyo nyama ya nguruwe kufuatia kufumuka kwa ugonjwa wa homa ya nguruwe (African swine fever) nchi jirani ya Malawi.

Mkuu wa mkoa huo, John Mwakipesaile alitoa agizo hilo alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema ugonjwa huo uliibuka nchini Malawi kwenye wilaya ya Karonga inayopakana na wilaya ya Kyela na kwamba tayari umeingie nchini na kuua nguruwe 328 katika wilaya za Rungwe na Kyela.

Dalili za ugonjwa huo ni nguruwe kupata joto la kutoka nyuzi joto 30 la kawaida hadi kuwa zaidi ya 40 na baada ya hapo nguruwe wanajikunyata pamoja na kuonyesha udhaifu.

Mkoa wa Mbeya una jumla ya nguruwe 150,070, ambapo kwa Wilaya ya Kyela wapo 32,000 na Rungwe inao nguruwe 56,000.

Mwakipesile alisema ugonjwa huo umebainika nchini takribani wiki moja baada ya kutokea tishio la ugonjwa huo katika nchi jirani ya Malawi ambayo tayari imeweka

karantini ya kusafirisha wanyama hao.

Alisema kupitia vikao vya ujirani mwema ambavyo vinaambatana na kubadilishana taarifa, serikali yake ilipata taarifa za kulipuka kwa ugonjwa huo hatari kwa afya za nguruwe, ambapo mbali ya kuathiri wanyama hao lakini pia ni hatari kwa afya za binadamu.

Alisema ofisi yake imepata taarifa kutoka kwa wataalamu wa Wilaya ya mpakani ya Karonga juu ya kulipuka kwa ugonjwa wa homa ya Nguruwe hivyo kuchukua tahadhari na baada ya wiki moja wataalamu wa Wilaya za Rungwe na Kyela nao wakabaini kuwepo kwa homa.

Aidha, alisema kwa mujibu wa taarifa alizozipata kutoka nchini Malawi, serikali ya nchi hiyo iliamuru kuendesha zoezi la kuteketeza nguruwe wote katika Wilaya ya Karonga iliyopo kusini mwa nchi hiyo ambayo inapakana na Tanzania kwa Wilaya ya Kyela.

Kwa upande wake mganga wa mifugo wa mkoa huo, Dk Solomon Ng'ong'ona alisema kuwa licha ya ugonjwa huo kutokuwa na madhara yoyote kwa binadamu, lakini alishauri watu kutobweteka kwa kula nyama ya nguruwe ambaye amepatwa na ugonjwa huo.

Ng'ong'ona alisema ugonjwa huo hauna tiba wala kinga na kwamba mbali na madhara ya kiafya kwa wanyama hao,lakini pia ni hatari kwa madhara ya kiuchumi kwa kuwa wafugaji huweza kupoteza mifugo yao hiyo kama hawatachukua hatua za kudhibiti.